**KAULI YA SERIKALI KUHUSU WANAFUNZI WA DIPLOMA MAALUM YA UALIMU WA SAYANSI WALIORUDISHWA NYUMBANI**

**Mheshimiwa Spika,**

Leo Tarehe 30 Mei, 2016 baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu, uliniagiza nitoe maelezo ya Serikali kuhusu sababu za wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao wameelekezwa na Uongozi wa Chuo Kurudi nyumbani kutokana na mgomo wa Wahadhiri wanaofundisha kozi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Wahadhiri wa Chuo Kikuu Dodoma wanaofundisha diploma ya ualimu wa Sayansi walianza mgomo tarehe 9 Mei, 2016 kutokana na kudai malipo ya muda wa ziada wanaoutumia kuwafundisha wanafunzi wa Kozi Maalum ya Diploma ya Ualimu wa Sayansi. Madai hayo

yalipohakikiwa yalionekana kuwa yalikuwa juu kuliko wanavyostahili, kwa mujibu wa Sera ya Chuo ya Uzito wa Kazi (University Workload Policy). Kiasi kilichowasilishwa kilikuwa Shs. **934,551,500** wakati kiasi kilichohakikiwa kilikuwa ni Shs. **252,120,000** ambacho wahadhiri hawakikubali.

**Mheshimiwa Spika,**

Jitihada za kupata ufumbuzi wa mgomo wa wahadhiri zilifanyika ambapo tarehe 19 Mei, 2016 Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Eng. Stella Manyanya (Mb.) na Naibu Katibu Mkuu walienda Chuoni kwa lengo hilo la kupata ufumbuzi.

Aidha, tarehe 26/04/2016 Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Naibu Katibu Mkuu walifika tena katika Chuo Kikuu cha Dodoma kwa lengo hilo hilo la kupata ufumbuzi. Hata hivyo jitihada zao hazikuweza kuzaa matunda.

Kutokana na hali ya Wahadhiri kutokufundisha kwa zaidi ya wiki 3 na wanafunzi kutokufudishwa na hivyo kuzua hali ya wasiwasi chuoni, Uongozi wa Chuo Kikuu Dodoma umeona ni vema wanafunzi hao warudi nyumbani kwao wakati hatua za kupata ufumbuzi wa suala hili zinaendelea kuchukuliwa. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Uongozi wa Chuo itapitia mfumo wa utoaji wa mafunzo hayo na kuangalia utaratibu mzuri zaidi ambao utakuwa na tija kwa wanafunzi, Wahadhiri na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, tarehe 06 Aprili, 2016, Bodi ya Mikopo ilitoa kiasi cha Shs.3.9 bilioni kama

Fedha za kujikimu kwa ajili ya wanafunzi hao. Aidha kwa mujibu wa taarifa ya Makamu Mkuu wa Chuo cha Dodoma, tarehe 21 Aprili, 2016 wanafunzi hao walilipwa Fedha zao za kujikimu ambazo zilikuwa ni za matumizi kwa muda wa siku 60.

**Mheshimiwa Spika,**

Dhamira ya Serikali ni njema kuhakikisha kuwa changmoto zote zinazohusiana na kazi hiyo maalum zinapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Napenda kutoa wito kwa Wanafunzi, Wahadhiri, Wazazi na Walezi kwa ujumla kuvuta subira wakati Serikali inalifanyia kazi suala hili.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.